# HUTUBA YA MHESHIMIWA LELA MUHAMED MUSSA KATIKA UFUNGUZI WA MKUTANO WA SABA WA TATHMINI YA SEKTA YA ELIMU

**MADINAT AL BAHR, MBWENI ZANZIBAR**

**16TH APRIL 2024**

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali,
Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi,
Katibu Mtendaji Tume ya Mipango,
Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali,
Manaibu Katibu Wakuu; Utawala na Taaluma Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali,
Wakuu wa Vyuo Vikuu
Wenyeviti wa Bodi za Taasisi za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali,
Viongozi Wastaafu
Wakurugenzi,
Washirika wa Maendeleo
Wawakilishi wa Asasi za Kiraia,
Wadau wa Elimu wa Sekta Binafsi
Wazazi,
Walimu na Wanafunzi,
Waandishi wa Habari
Mabibi na Mabwana

**Assalamu Alaikum,**

**Ndugu washiriki,** awali ya yote hatunabudi kumshukuru muumba wa mbingu na ardhi bwana wa viumbe vyote ulimwenguni kwa kutuwezesha kushiriki katika mkutano huu wa saba wa tathmini ya sekta ya elimu tukiwa na wingi wa afya njema na amani iliyotawala katika kila kona ya visiwa

vyetu. Hakika ni kwa uwezo na mapenzi yake tu yamefanya tuwe sehemu ya washiriki wa mkutano huu. Aidha nichukuwe fursa hii kuwashukuru nyote muliojumuika katika mkutano huu. Licha ya kuwa na majukumu mazito katika taasisi zenu mumefanikiwa kutenga muda wenu na kuamua kushiriki katika mkutano huu wa tathmini ya sekta ya elimu nchini. Kutokana na kutambua umuhimu wa mkutano huu baadhi ya wadau ambao wamesindwa kufika hapa moja kwa moja wameamua kujumuika na sisi kwa njia ya mtandao. Hii inadhihirisha utayari wenu katika kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuimarisha sekta ya elimu nchini. Kwa upande wetu kama Serikali tunathmini mchango wenu na hivyo tunawaahidi kuendelea kushirikiana kuhakikisha kuwa watoto wetu wanapata elimu iliyobora.

**Ndugu washiriki,** kwa kipindi cha miaka saba mfululizo sasa mkutano huu umekuwa ni jukwaa linalotoa fursa kwa wadau mbali mbali wa sekta ya elimu kushiriki katika mijadala ya kutathmini maendeleo ya sekta kwa kipindi cha mwaka uliopita na kuandaa mustakbali wa sekta kwa kipindi cha mwaka unaofuata. Kwa kutambua umuhimu wa mkutano huu, Serikali haikuwahi kusita kufanya mikutano hii kila mwaka tokea pale tulipoanza kwa mara ya kwanza mwaka 2018. Utekelezaji wa mikutano hii ni kielelezo tosha cha Serikali inayozingatia misingi ya utawala bora katika kuwaongoza na kuwaletea maendeleo wananchi wake katika nyanja mabli mbali ikiwemo sekta ya elimu. Hili linadhihirishwa si tu kwa ushiriki wenu katika makundi mbali mbali yakiwemo Wanasiasa, Washirika wa Maendeleo, Asasi za Kiraia, Taasisi za Serikali, Walimu, Wazazi na Wanafunzi bali pia na fursa inayopatikana katika mkutano huu ya kichangia mada mbali mbali kwa uwazi wa hali ya juu. Utamaduni huu umeisaidia Serikali kuibua hoja za msingi na kuzifanyia kazi na hivyo kwa

namna moja ama nyengine mikutano hii imekuwa ni jukwaa linalochagiza mafanikio ya sekta tunayoyashuhudia.

**Ndugu washiriki,** mwaka 2022 jamii ya Kimataifa ilianza safari ya mabadiliko ya mifumo yetu ya elimu, mpango ambao uliafikiwa kwa pamoja katika Mkutano wa Mabadiliko ya Elimu “Transforming Education Summit” uliofanyika nchini Marekani. Katika mkutano huo Mataifa kutoka kila pembe ya Dunia yaliungana kwa dhamira moja tu ya kuipitia upya mifumo yetu ya elimu ili iweze kukidhi mahitaji ya maendeleo endelevu. Katika kuitikia wito huu wa Kimataifa, Jamuhuri ya Muungano ya Tanzania kwa kuzingatia umuhumimu wa kuihusisha elimu na changamoto za karne ya 21 ilitangaza nia yake ya kuanza safari ya mageuzi ye elimu kwenye maeneo makubwa matano. Zanzibar ikiwa kama sehemu ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania iliunga mkono ahadi hii kwa hatua madhbuti. Katika mwaka huo huo wa 2022, Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali iliunda kikosi kazi kwa lengo la kuupitia vyema mfumo wetu wa elimu na kuweza kupendekeza maeneo yanayostahili kufanyiwa mageuzi. Itakumbukwa kuwa kazi hii ilifanywa kwa uweledi mkubwa na kufanikiwa kupata mapendekezo mbali mbali ambayo yamegaiwa katika maeneo makuu nane ya mageuzi. Kitu cha kujivunia ni kuwa maeneo haya nane yanalingana moja kwa moja na maeneo matano ambayo Tanzania imeahidi katika Jamii ya Kimaifa kuyafanyia kazi katika kuleta mabadiliko kwenye mifumo yetu ya elimu.

**Ndugu washiriki,** pamoja na kwamba tumeweka misingi na ahadi za mageuzi ya elimu, safari ya kufikia meguzi hayo ni ndefu. Mikakati tuliyoiweka kwamwe haiwakilishi mwisho wa mageuzi bali ni mwanzo wa

safari ambayo inahitaji kujitoa kwa kila mmoja wetu. Tukiwa kama wasimamizi wa ajenda hii ya mageuzi, tunawajibika kuhakikisha urasimu hauchukuwi nafasi katika utekelezaji wa mapendekezo hayo bali mapendekezo hayo yanatafsiriwa kivitendo na athari zake kuonekana katika madarasa na jamii kwa ujumla. Lengo letu ni kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa Zanzibar inaendana na mahitaji ya karne ya 21, kwa kuzalisha vijana wenye uwezo wa kufikiri kwa kina, kutatua matatizo, na kuwa na uwezo wa kushindana katika soko la ajira la dunia. Tunaamini kwamba kwa kuandaa vijana wenye ujuzi na maarifa, tunachangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa taifa letu, na hivyo kufikia malengo tuliyojiwekea katika Dira ya Maendeleo ya 2050. Ni katika muktadha huu kwa pamoja tumeamua mkutano huu ujikite katika maudhuwi ya ***"Mageuzi ya Elimu kwa Maendeleo Endelevu".*** Kwa maudhuwi haya tutapata fursa ya kutafakari kwa pamoja juu ya hatua tulizopiga tokea kuanza kwa safari yetu ya mabadiliko, kutambua changamoto zinazotukabili na zilizo mbele yetu katika utekelezaji wa mageuzi hayo lakini hatimae tuweze kuweka mikakati itakayowezesha utekelezaji mzuri wa mageuzi hayo.

**Ndugu washiriki,** kwa upande wa Serikali tumeweza kuchukuwa hatua mbali mbali katika kufanikisha adhma ya kuujenga mfumo wetu wa elimu katika namna ambayo inaakisi mahitaji yetu na ya kiulimwengu kwa ujumla. Sisi sote ni mashuhuda, ngazi ya elimu ya maandalizi na msingi tumeanza kutumia mtaala mpya ambao unalenga kuwajengea watoto wetu ujuzi na maarifa badala ya ufahamu. Aidha kwa upande wa ngazi ya elimu sekondari tumeanza majaribio ya mtaala mpya wa ngazi hiyo katika skuli ya Sekondari ya Mwanakwerekwe. Kwa sababu mageuzi hayagusi ngazi za chini peke yake, tayari taasisi za elimu ya juu nchini zimeanza

mchakato wa kuipitia mitaala yao ili iweze kuendana na dhamira ya Serikali. Ni matarajio yetu kuwa utekelezaji wa mitaala hii mipya itatengeneza msingi Madhubuti wa kuyafikia malengo ya mageuzi ya mifumo yetu ya elimu nchini.

**Ndugu washiriki,** ni Dhahiri kuwa utekelezaji wa mitaala hii pamoja na dhana nzima ya megeuzi inahitaji miundombinu ya kisasa na ya kutosha. Kwa kulitambua hili na kwa kuzingatia changamoto inayotukabili ya msongomano wa wanafunzi kwa darasa pamoja na uendeshaji wa skuli zetu katika mtindo wa shifti, Serikali imedhamiria kuondosha kadhia hii ili kuwezesha watoto wetu kuweza kupata elimu katika mazingira bora. Katika kipindi cha miaka mitatu ya uwongozi wa Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Serikali imefanikiwa kujenga jumla ya madarasa 2,273 pamoja na vyoo 2,189. Sambamba na ujenzi wa madarasa, Serikali pia imeweza kujenga maabara, dakhalia na nyumba za walimu. Ni matumaini yetu kuwa kasi hii ya uimarishaji wa miundombinu itasaidia kuondokana na changamoto hiyo ndani ya kipindi kifupi kijacho. Aidha, katika kuhakikisha uzimamizi mzuri wa utoaji wa elimu nchini kupitia mapendekezo mulioyatoa katika mkutano kama huu mwaka jana, Serikali imefanikiwa kujenga ofisi maalumu za Elimu za Wilaya. Jumla ya ofisi saba za elimu za Wilaya zimejengwa katika Wilaya ya Mjini, Magharibi B, Kati na Kaskazini A kwa Unguja na kwa upande wa Pemba; Wilaya ya Wete, Chake Chake na Mkoai. Wizara imepanga kumalizia ujenzi wa ofisi nyengine nne ili kuifanya kila Wilaya kuwa na ofisi yake. Haya ni mageuzi makubwa katika mfumo wa elimu na kila mmoja wetu anapaswa kujivunia hatua hii.

**Ndugu washiriki,** wakati juhudi za uimarishaji wa miundombinu zikiendelea, kwa upande mwengine Serikali ipo katika hatua za mwisho za ukamlishaji wa mpango wa utekelezaji wa mageuzi ya elimu utakaotekelezwa kwa kipindi cha miaka saba hadi 2030. Kukamilika kwa mpango kutatoa fursa ya kufuatilia kwa ufanisi utekelezaji wa mapendekezo tuliokubaliana. Na kwa kutumia jukwaa hili kila mwaka washiriki watakuwa na fursa ya kupima utekelezaji wa mpango huo kupitia viashiria vitakavyowekwa. Kupitia mpango huu pamoja na mambo mengine Serikali imetoa mkazo katika uimarishaji wa ujuzi kwa wanafunzi wetu hivyo suala la elimu ya ufundi na mafunzo ya amali litakuwa na nafasi kubwa katika utekelezaji wa mpango huo. Tunatarajia kushuhidia ujenzi mkubwa wa vyuo vya amali pamoja na skuli za ufundi. Maeneo mengine yaliyopewa kipaumbele katika mpango huo mutapata fursa ya kuyaona wakati wa uswasilashi wa mpango huo kwani nimearifiwa mpango wa sekta utakuwa ni moja wapo ya mawasilisho katika mkutano huu. Aidha, Serikali inatambua kuwa pamoja na kuwa na mipango huo ni lazima mchakato wa mapitio wa Sera na Sheria ya elimu uwe umekamilika ili kuandaa mazingira bora ya utekelezaji wa mpango huo. Kwa kutambua umuhimu wa suala hili Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo tupo katika hatua za mwishoni kumalizia rasimu ya Sera ya Elimu ambayo itaendana na mapendekezo yalioainishwa katika repoti ya mageuzi ya elimu.

**Ndugu washiriki,** munaweza kuona ni kwa kiasi gani Serikali ilivyodhamiria kwa vitendo kuyafikia mageuzi ya elimu kwa mustakbali wa vizazi vyetu na Taifa kwa ujumla. Hivyo, ni jukumu lenu kupitia jukwaa hili kuweza kutafakari maeneo ambayo munahisi bado hatajaweza kuyagusa ipasavyo pamoja na kutashauri namna bora ya kuweza kutekeleza

mapendekezo hayo. Tufanye hivyo kwa kutambua kuwa suala la elimu si suala la mtu mmoja bali ni sekta ambayo inamgusa kila mtu na kila nyanja ya maisha yetu. Uwepo wetu hapa leo katika makundi mbali mbali ni ushahidi wa hayo. Ni matarajio yetu kuwa mutatumia vizuri uzoefu mulioupata wakati wa ziara za taasisi mbali mbali za elimu zilifanyika mwezi Machi pamoja na mwasilisho yatakayofanywa katika mkutano huu ili kuweza kutoa maazimio ambayo yatakuwa chachu ya utekelezaji wa mageuzi ya elimu nchini.

**Ndugu washiriki,** Kabla ya kuhitimisha hutuba yangu, ningependa kutumia fursa hii kuwahakikishia kwamba tutaendelea kushirikiana kwa karibu katika kuhakikisha sekta ya elimu inaimarika zaidi. Ushirikiano huu hautaishia hapa tu katika mkutano huu, bali utaenea katika kila eneo ambalo linahusu maendeleo ya elimu katika nchi yetu. Nawashukuru kwa mara nyengine tena kwa kujumuika nasi katika mkutano huu muhimu. Aidha ningependa kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati kamati ya maandalizi ya mkutano kwa kazi nzuri waliyoifanya kuufanikisha mkutano huu. Pia, nawatakia washiriki wote mafanikio katika majadiliano yetu. Ni matumaini yangu kwamba mkutano huu utakuwa wa mafanikio makubwa na utatoa mapendekezo muhimu ya kuimarisha sekta yetu ya elimu. Kwa haya machache, natamka kuwa mkutano wa saba wa tathmini ya sekta ya elimu Zanzibar kwa mwaka 2024 umefunguliwa rasmi!

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**